**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA-TAMISEMI**


**SHULE YA SEKONDARI MZENGA,**
**S.L.P 28021,**
**KISARAWE – PWANI.**

**KATA YA VIHINGO**
**SIMU NA: +255752885600 MKUU**
**SIMU NA: +255621835302 MAKAMU**
**Email: mzengasec@gmail.com.**


# MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MZENGA KIDATO CHA TANO

Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi,

**…………………………………………....** (Majina matatu ya Mtoto)

**S.L.P ………………………………….,**

**MJI…………………………………….**

**Ndg,**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao ni miongoni mwa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha tano shule ya Sekondari ya Mzenga Tahasusi ya **…………..** kwa mwaka wa masomo **2026/2027**.
Ninampongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na shule hii, Hongera sana!
Ni matumaini yangu kuwa ataipokea kwa furaha na kuitumia nafasi hii kujiendeleza kielimu kwa manufaa yake binafsi, familia yake na taifa kwa ujumla.

Yafuatayo ni mambo anayotakiwa kuyatimiza kabla ya kujiunga na shule ya Sekondari Mzenga; -

## 1. KUFUNGUA SHULE.

Shule itafunguliwa rasmi mnamo tarehe ……… naye anatakiwa kufika mnamo tarehe **……..** siku ya **Jumatatu** tayari kuanza masomo rasmi. Na mwisho wa kuripoti ni Tarehe **…………..**
Kutokufika shule kwa muda huo ni kosa na utakuwa umepoteza nafasi hiyo, hivyo basi zingatia kufika kwa wakati ili ukamilishe usajili.

## 2. MAHALI SHULE ILIPO.

Shule ya Sekondari Mzenga ipo katika Kijiji cha **Mzenga B,** kata ya **Vihingo,** tarafa ya **Mzenga,** kando kando mwa barabara itokayo **Mlandizi** kwenda **Maneromango.**

**JINSI YA KUFIKA SHULENI:**

Watakao pita Barabara ya **Morogoro**, washuke **Mlandizi** na waulizie stendi ya magari yanayoelekea Mzenga.

Kutoka **Mlandizi** hadi **Mzenga Sekondari** kuna umbali wa kilomita **25** na shule ipo kando ya Barabara, na nauli kwa gari **Tsh. 4,000/=** na pikipiki ni **Tsh. 6,000/=**

Atakaetokea **Dar es Salaam,** Aende hadi **stendi ya Kigogo fresh Chanika,** ataulizia magari ya Mzenga na atashukia **Mzenga A** nauli ni Tsh. 7,000/= kisha utachukua bodaboda itakuleta Mzenga Sekondari, nauli 1,000/= AU njia nyingine kwa atakaetokea Dar es salaam, afike stendi ya Mbezi kisha ataulizia magari ya Mlandizi na atashuka Mlandizi na kisha ataulizia stendi ya Mzenga.

## 3.1. SARE RASMI YA SHULE AMBAYO INAPATIKANA KWENYE MASOKO MBALIMBALI (SIO SHULENI)

***WAVULANA***

a) Shati Nyeupe yenye mikono mirefu jozi 2, liwe na mfuko mmoja.

b) Suluari za **Kijivu Mpauko (Escot Grey)** jozi 2, ziwe na rinda mbili na mfuko mmoja wa nyuma na chini nchi 16 Upana. Kuvaa modo (model) au Mlegezo ni Kosa.

c) Viatu Vyeusi vya ngozi vya kufunga kamba jozi 2 (**Gidamu**) na visiwe na visigino virefu vya kupiga kelele sakafuni.

d) Bukta moja ya rangi ya **Blue** na Fulana ya Jezi ya taifa rangi ya ***Blue,*** kwa ajili ya michezo.

e) Soksi za Rangi Nyeusi pair 3.

f) Shamba Dress (nguo za kushindia) suluari Nyeusi za kitambaa 2 (sio Kadeti)

g) Track Suit ya **Kijivu (Escot Grey)** kwa ajili ya preparation au Masomo ya usiku.

h) Raba rangi nyeupe za michezo

i) Kanda mbili za rangi ya **BLUE (Sio Yeboyebo Wala Sendos)**

***WASICHANA.***

(a) Shati Nyeupe yenye mikono mirefu jozi 2 yenye mfuko mmoja.

(b) Wasichana wa Kiislamu, watashona nusu kanzu ambayo wataivaa na hijabu nyeupe iwe ndefu hadi vidole vya mikono.

(c) Sketi za **Kijivu Mpauko (Escot Grey)** jozi 2, ziwe na mshono wa umbo la V na ziwe ndefu hadi kwenye fundo za miguu

(d) Viatu Vyeusi vya ngozi vya kufunga kamba jozi 2 (**Gidamu**) na visiwe na visigino virefu vya kupiga kelele sakafuni.

(e) Bukta moja ya rangi nyeupe na Fulana ya **jezi ya taifa rangi *nyeupe,*** kwa ajili ya michezo.

(f) Soksi za Rangi Nyeupe pair 5 au zaidi.

(g) Shamba Dress (nguo za kushindia) ni G**AUNI** ya kijani drafti ndogo iwe ndefu hadi kwenye fundo za miguu, mikono mirefu au mikono mifupi ya kufika kwenye kiwiko cha mkono (**SIO VEST STYLE**)

(h) Track Suit ya **Kijivu (Escot Grey)** kwa ajili ya preparation au masomo ya usiku.

(i) Hijabu ya rangi ya kijani kwa ajili ya kushindia.


(j) Raba rangi nyeupe za michezo

(k) Kanda mbili rangi ya BLUE (sio yeboyebo wala sendos)

**Mfano wa sare ya darasani (was & wav)**



**mfano wa gauni la kushindia (wasichana tu)**



**3.2. SARE AMBAZO ZINAPATIKANA SHULENI**

a) Tshirt ya shule yenye kola ya rangi ya kijivu mpauko (**Escort Grey)** yenye nembo jozi 2 ni lazima inavaliwa kama sare siku ya Juma tano na Ijumaa na pia kushindia. (**Inapatikana shuleni kwa Tsh. 15,000/=)**

b) Sweta la shule lenye nembo rangi ya kijivu mpauko (**Escort Grey)** huvaliwa nyakati za baridi darasani. ( **inapatikana shuleni kwa Tsh. 15,000/=)**

c) Nembo ya shule

**ZINGATIA:** Nguo ambazo siyo sare ya shule haziruhusiwi shuleni. Ukaguzi wa vifaa na vitu vyote vitakavyoletwa shuleni utafanyika. Ukipatikana na vifaa/nguo zisizohitajika utalazimika kuzirudisha nyumbani.

**Mwanafunzi aripoti shuleni akiwa amevaa sare ya shule**.

**4.1. MAHITAJI MUHIMU KWA MATUMIZI YA USAFI**

a. Ndoo ndogo 1 ya kuogea ya lita 10
b. Ndoo kubwa 1 lita 20 kwa matumizi ya shule.
c. Wavulana tahasusi ya HGK wataleta Jembe na mpini wake, Fagio laini (soft blooms), Sabuni ya maji lita 5
d. Wasichana tahasusi ya HGK wataleta Panga, Fagio ngumu (hard blooms), Dawa ya chooni lita 5
e. Wavulana tahasusi ya HGLwataleta Kwanja, Reki, Squeezer.
f. Wasichana tahasusi ya HGL wataleta Jembe na mpini, Fagio ngumu (hard blooms), Squeezer.

**4.2. MAHITAJI MUHIMU KWA MATUMIZI BINAFSI NA SHULE.**

a) Madaftari Makubwa **7** QUARE 4.

b) Kalamu za Wino 4 (blue au nyeusi) na Kalamu za Risasi 2 (penseli) aina ya HB.

c) Seti ya Vifaa vya Hisabati 1 (Mathematical Set) kwa wataosoma somo la Geography.

d) Bunda mbili za Karatasi, moja (**Ream A4** aina ya **Smart Copy)** na moja ya mistari **(Ruled)** kwa kila nusu muhula kwa ajili ya mitihani ya mara kwa mara.

e) File (**spring file transparent**) la kuwekea taarifa za mwanafunzi.

f) Picha mbili za passport size za Mwanafunzi na mbili za Mzazi au Mlezi zibandikwe kwenye fomu

g) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika orodha imeambatanishwa mwishoni mwa fomu hii.

h) Scientific Calculator; kwa watakaosoma somo la Geography.

i) Godoro futi 2.5

j) Mashuka Jozi 2 rangi ya pink (kwa wasichana) na light blue (kwa wavulana), blanket

k) Foronya ya godoro 1 rangi ya shuka lako, chandarua 1 ya pembe 4 rangi nyeupe size ya futi3.

l) Nguo za ndani za kutosha;

m) Vyombo vya chakula sahani, bakuli, kikombe ziwe za mfupa zisiwe za mpila (plastic) kijiko na chupa ya kuhifadhia maji ya kunywa.

n) Ni lazima mwanafunzi kuja na kadi ya bima ya afya au aje na tsh. 50,400/= kwa ajili ya bima ya afya kwa matibabu ya mwaka mzima (NHIF). kadi ya bima afya itakaguliwa au pesa itapokelewa siku ya kuripoti.

o) Fedha za kutosha za matumizi binafsi ya mwanafunzi kwani hakuna fursa kupiga simu mara kwa mara.

## 5. MICHANGO MBALIMBALI

**Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB:** Michango ilipwe Benki ya NMB tawi lolote la NMB.

- Akaunti Namba: **21401100005**
- Jina la Akaunti ni**: MZENGA SECONDARY SCHOOL.**

**ANGALIZO:** kwenye risiti ya malipo, andika majina ya mwanafunzi, siyo ya mzazi na uje na risiti ya malipo siku ya kuripoti.

## 6. UHURU WA KUABUDU.

Utaruhusiwa kuabudu kwa kufuata sheria, ratiba na taratibu za shule na za nchi

## 7. KUWATEMBELEA WANAFUNZI/SIKU YA WAGENI SHULENI.

Wazazi/walezi wataruhusiwa kuwatembelea wanafunzi mara moja kwa muhula kwa tarehe itakayopangwa itakuwa siku ya Jumamosi kuanzia saa 4.00 asubuhi mpaka 10.00 jioni. Matron na Patron watakuwepo kuonana na wazazi ili kujadiliana kuhusu maswala ya kitaaluma na nidhamu ya mwanafunzi. Hairuhusiwi kumletea mwanafunzi aina yoyote ya chakula. Aidha.

**Hairuhusiwi mwanafunzi kumiliki simu, line, au chaja akiwa shuleni wala kuletewa na mzazi siku anapotembelewa shuleni, ikibainika hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa.**

**8. MPANGO WA USAFIRI.**

Mpango wa Usafiri. Unapokuja na kurudi nyumbani wakati wa likizo utajilipia nauli ya usafiri wakufika Mzenga. Mwalimu wa usafiri atakusaidia kufanya mpango wa usafiri wakati wa kwenda na kurudi likizo. Mzazi unatakiwa kumlipia mtoto wako nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani mapema, ili mipango ya usafiri ifanyike mapema. Ni lazima mwanafunzi asafiri na gari ilioandaliwa na shule, na asafiri akiwa amevaa sare ya shule kila anapokwenda nyumbani na kurudi shuleni

**9. VITU VISIVYORUHUSIWA SHULENI.**

(a) Simu za mkononi (charger, line za simu, vocha na vyote vinavyoendana na simu) Mawasiliano muhimu baina ya mzazi/Mlezi na mwanafunzi yafanyike kupitia kwa Mkuu wa Shule kwa anuani tajwa hapo juu.
(b) Pasi za umeme, heater, birika la umeme
(c) Kusuka nywele au kuweka dawa za aina yoyote ile
(d) Kupaka rangi kucha au kupaka ina, wanja na lipstic
(e) Nguo za nyumbani zisizo sare ya shule.
(f) Heleni, Mkufu, pete na bangili.
(g) Vitu vyenye ncha kali kama vile kisu, panga na vitu vingine mfano wa silaha
(h) Dawa za aina yeyote hadi uwe na kibali cha daktari na kuthibitishwa na Matron au Patron.

**10. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, sayansi, na teknolojia yenye dhamana ya elimu chini ya ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni na asubuhi (preparation)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shuleni na nyingine utakazopewa
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
(i) Kutunza mali za umma
(j) Mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote awapo shuleni.
(k) Kusimama na kusalimia pale anapopita Mwalimu au mgeni yeyote.\
(l) Itika, wahi na kimbia pale unapopata wito wa Mwalimu au kusikia kengele.
(m) Ni marufuku kubaki bwenini muda wa vipindi na mara tu unaposikia kengele ya wito.

(n) Hairuhusiwi kukatiza viunga vya shule.

(o) Hairusiwi Kwenda kwenye nyumba za walimu.

**11.** MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA **KUFUKUZWA** AU **KUSIMAMISHWA** SHULE

(a) Wizi.
(b) Utoro
(c) Uasherati na ushoga.
(d) Ubakaji.
(e) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
(f) Kupigana na kupiga.
(g) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(h) Kudharau Bendera ya Taifa.
(i) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
(j) Kutoa mimba.
(k) Kuoa au kuolewa.
(l) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.
(m) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(n) Kuwa na simu ya mkononi.

**12. MAMBO MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.**

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wakutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

d) Nakala au kivuli ya cheti cha kuzaliwa mwanafunzi.

e) Nakala ya matokeo ya kidato cha nne **(Result Slip).**

f) Bima ya afya NHIF ni lazima kama mwanafunzi hana bima aje na 50400/= kwa ajili ya kukata bima, bila bima ya afya ya NHIF mwanafunzi hatapokelewa.

g) Risiti ya malipo ya benk ya NMB

Mwisho, Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MZENGA**

**............................**

**HASSAN RASHID RUSHEYE**

**MKUU WA SHULE**

**SIMU; 0716914523 /0752885600**

PRIME MINISTER'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT - RALG

KISARAWE DISTRICT COUNCIL

Mzenga Secondary school

P.O.BOX 28021 KISARAWE - PWANI.

MEDICAL EXAMINATION FORM

To Medical Officer

................................................

RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF STUDENT

Student Name.................................................................

Please examine the above named student as to his / her fitness for appointment as a student. Comment on his / her health responding to the following items

A. Sight.......................................................................................................................
B. Hearing...................................................................................................................
C. Speech....................................................................................................................
D. Blood pressure.......................................................................................................
E. Asthma....................................................................................................................
F. T.B...........................................................................................................................
G. Stool examination.................................................................................................
H. Pregnancy (Girls only) .........................................................................................
I. Height (cm).............................................................................................................
J. Weight (kg) .............................................................................................................

**Additional information** if any ) e.g. Physical defects, impairment(s) e.g. arm, leg etc. infection chronic or family disease etc.

..............................................................................................................................................................

..............................................................................................................................................................

I have examined the student and consider that he/she is physically fit/unfit to pursue school activities.

Signature.............................................................. Date...........................................

Designation......................................................... Station stamp..............................

OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA - TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE

# Shule ya Sekondari Mzenga

PASSPORT YA MWANAFUNZI

PASSPORT YA MZAZI/MLEZI

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MZENGA

1. Jina kamili la mwanafunzi……………………………………………………………………..

Tarehe ya kuzaliwa………………Mwezi…………Mwaka…………..……..

Wilaya uliyozaliwa…………………………………. Mkoa…………………………………

Uraia…………………………………………… Dini……………………………………..

Shule ya Sekondari uliyotoka……………………………… Daraja la ufaulu: ……… Alama ……..

Jina kamili baba………………………………………………………………………………
Wilaya aliyozaliwa. ……………………………….....Mkoa. ……………………………………..
Uraia ……………………………… Dini. ……………………………………………………….
Namba ya nida (nin) ya baba………………………………………………………………..

Jina kamili la mama. ……………………………………………………………………..
Wilaya aliyozaliwa …………………………………..Mkoa ………………………………………
Uraia …………………………………… Dini ………………………………………………….
Namba ya nida (nin) ya mama. ……………………………………………………………….

Je, wewe unaishi na nani? Jina **(Unaeishi Nae)** ……………………………………………………………………………………

Uhusiano (taja)

Anuani

______________________________________________________________

Je, uliwahi kuwa kiongozi? Ndiyo/Hapana

Kama ndiyo taja nafasi ilikuwa ipi? ____________________________________________

________________________________________________________________________

Utakuwa unakwenda wapi wakati wa likizo………………………………………

(Wakati wa likizo unatakiwa kwenda kwa mzazi au mlezi aliyetajwa tu. Kama utabadilisha mahali pa kwenda likizo, mzazi/mlezi atoe idhini kwa maandishi mwezi mmoja kabla)

**AHADI YA MZAZI/MLEZI/ NA MWANAFUNZI**

Mimi (Jina kamili la mzazi)____________________________________________________________

Anuani

________________________________________________________________________

Simu

___________________________________________________________________________

Mzazi/Mlez(tajauhusiano)

_____________________________________________________________________

Nakubali mtoto wangu (Jina lake) ____________________________________________________

1. Asome katika shule ya Sekondari ya Mzenga, kadiri alivyopangiwa.
2. Nimempa fedha ya mahitaji inayotakiwa na nitashirikiana na walimu katika suala zima la malezi ya mwanangu na maendeleo yake kitaaluma na kumsaidia mtoto kufuata sheria za shule.

Jina (Mzazi/Mlezi)______________________________________________________________

Saini ______________________________________________________________________

Tarehe____________________________________________________________________

Namba ya simu____________________________________________________________

Namba ya simu yenye **WhatsApp** ya kwako au miongoni mwa ndugu wa Mwanafunzi walioonyeshwa kwenye Form hii.

Mimi ___________________________ (Jina la Mwanafunzi) nimekubali nafasi hii, naahidi kufuata sheria za shule na kuwatii walezi na wakubwa, tena nitafanya bidii ya kujifunza ili nifaulu vyema masomo yangu.

Saini ____________________________________________________________________________

Tarehe_

## OORODHA YA VITABU

### SOMO LA GEOGRAPHY

1. Physical Geography by TIE.
2. Practical Geography by TIE.
3. Principles of Physical Geography by F J Monk House
4. Geography Integrated Approach by D. Waugh
5. Essentials of Practical Geography by Josephat Mwita
6. General Geography in Diagram by R.B Burnet
7. Simplified Physical Geography(A-LEVEL) by D M
8. Statistical Methods and the Geographers by S. Gregory

### SOMO LA HISTORY

**1.** Advanced level History 1 by TIE.
**2.** Advanced level History 2 by TIE.
**3.** Advanced learners, History form V and six (history 1 and 2) (oxford 2011)
**4.** Advanced level History for Africa, From Neolithic Revolution to Present (zist Kamili 2010)
**5.** Major events in the World History
**6.** Advanced level History (Nyambari nyangwine 2007
**7.** Focus on Modern world history by Japhace, Ponsian, Chakupewa, Mpandije Yusuph P Maunda (2012

### SOMO LA ENGLISH LANGUAGE NA LITERATURE IN ENGLISH

1. English for Advance Level, Phonology, Stylistics
2. English for Advance level by TIE.
3. **Novel:** The Beautiful ones are not yet born, A man of the People, Divine Providence, His Excellency the Head of State, A season of Waiting, The Rape of the Pearl, Encounters from Africa
4. **Poetry:** Selected Poems, The Wonderful Surgeon and other Poems
5. **Plays:** an enemy of the People, Black Mamba, I will Marry When I want, Betrayal in the City, The Bride, Lwanda Magere

### SOMO LA KISWAHILI NA FASIHI YA KISWAHILI

1. **Kiswahili kwa ajili ya kidato cha Tano na Sita by TIE**
2. Sarufi Muundo ya Kiswahili (SAMIKISA)
3. Fasihi na Sarufi Sekondari na Vyuo
4. **Riwaya**: Vuta n'Kuvute, Mfadhili, usiku utakapokwisha, Kufikirika, Mfadhili.
5. **Tamthiliya**: kwenye ukingo wa thim, Morani, Kivuli Kinaishi, Nguzo Mama
6. **Ushairi**: Kimbunga, Chungu Tamu.Mapenzi Bora, Fungate ya Uhuru

### SOMO LA ACADEMIC COMMUNICSATION

### SOMO LA HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI